**Dondoo za Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**Tarehe 3 Novemba 2007**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Ally Salum
Aseli Wilison
Dominata Rwechungura
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Patrick Masinga
Paulo Atibu Hatibu
Protace Mugondo
Rahma Ali
Sudi Saidi Ramadhan
Yusufu Juma

**Msafara wa Baisikeli**
Elaine alisema anaandika repoti ya kuwapa Ubalozi wa Uholonzi na wadhamini wengine na anakaribia kumaliza. Wanachama wengine walimpa taarifa nyingine alizokosa. Kariu risiti zote za msafara zipo lakini tatu hazipo, na tutatoa photocopy.

Mabango kubwa zimepotea na Juma alizitafuta Mnazi Mmoja lakini wafanyakazi wa kule hawakuwa na taarifa.

Tuliweka picha za msafara kwenye bao za tangazo.

Sosthenes alipewa Tsh 30,000 na Elaine kufanya DVD ya msafara.

**Siku ya uamsho wa mabadalisho ya majira mwezi wa Desemba**
Elaine alisema kwamba tarehe ya siku ya uamsho wa mabadalisho ya majira itakuwa tarehe 8 Desemba. Atawasiliana na watu wa mashirikia mengine kama TANGO na mashirika ya mazingira kuangalia kama watashirikiana na sisi kuandaa. Baada ya hiyo tutaandika barua kwa Bwana Mengi kumpa taarifa na kumwalika.

Pia tutahitaji mabango kwa siku hiyo – tutaomba Sosthenes atengeneze.

**Ufuataliaji wa barua**
Juma alitembelea TANROADS na halmashauri ya Jiji kufuatalia majibu ya barua. Hatujapata jibu basi ataendelea kufuatalia.

**Ofisi**
Mejah alipendekeza mwanafunzi wa chuo anayeitwa Violeth kutafsiri taarifa na dondoo na ameshaanza kutafsiri dondoo.

Ally Saidi Mohammad alisema atatafuta bao laini zaidi kwa ajili ya bao za tangazo kwa sababu ni ngumu kuweka pini kwenya bao za sasa.

**Guta**
Jumanne na dereva wa guta walikuwepo kwenye mkutano. UWABA tunadai hela ya wiki nne kutoka dereva wa guta – wiki tatu za nyuma na wiki nyingine ambayo haijalipwa zamani. Guta halikutumiwa wiki jana kwa sababu ya kukosa kubalina na dereva wa guta. Tulikubali kwamba mwanachama mwingine wa kawaida awe dereva wa guta ambaye ataleta hela kila wiki. Jumanne alisema kama inatakiwa atalipa hela ya wiki mbili kutoka hela yake binafsi.

Hata hivyo, wanachama wengine hawakuwa tayari kufanya kazi ya udereva mpaka guta ina mpira mzuri zaidi. Kuna meli inaingia bandarini wiki hii na mpira mzuri. Basi guta alitatumikwa kwa wiki moja na tutachukua Tsh 90,000 kutoka benki kununua mipira mpya.

**Nyinginezo**
Elaine alisema hajapata mawasiliano kutoka Wamba Memorial fund kuhusu mradi wa usalama barabarani kwa wapanda baisikeli – atawatumia email wiki hii. Aidha mchango wa Italy haijafika benki kwa sababu ya shida za benki.

Tulizungumza kuhusu mataa ya baisikeli na Jumanne na Juma walipendekeza aina ya taa ya dynamo ambayo ni nzuri na zinapatikana wapi.

Wanachama walisema taarifa ya ajali za barabara haipo kwenye bao za tangazo na Elaine alisema ataleta wiki ijayo.